Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

### Una haki ya:

- kupokea maelezo kuhusu haki zako na kupata majibu kwa maswali yako
- kuteua mtu aliyeteuliwa
- kushirikiana katika kupanga mpango wako wa matibabu, msaada na kuruhusu
- ufaragha na usiri
- kufikia makumbukumbu yako ya uganga (haki hii inaweza kuwa na mipaka)
- maoni ya ziada kutoka mtaalum mwengine wa magonjwa ya akili – unaweza kumwombea mtaalum wako wa magonjwa ya akili, au Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili (s: 9222 4462) ili kupanga hiyo
- kufikia Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili (s: 1800 999 057). Mtetesi wa afya ya akili atakuwasiliana nawe bila kufikiri katika siku 7 (masaa 24 kwa watoto) baada ya wewe kuwa mgonjwa asiyekusudiwa
- kutoa malalamiko kwa huduma ya afya ya akili au Ofisi ya Malalamiko ya Huduma za Afya na Ulemavu (HaDSCO) (s: 1800 813 583).
- kupata kesi zako kukaguliwa rasmi na Baraza ya Afya ya Akili (s: 08 6145 3900). Baraza itapanga usikilizaji katika wiki 5 (siku 10 days kwa watoto) baada ya wewe kuwa mgonjwa asiyekusudiwa.

### Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake.

Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Maagizo ya matibu ya jamii



Agizo la matibabu ya jamii (Fomu 5A) ni agizo chini ya Sheria ya Afya ya Akili 2014 ili upokee matibabu kama mgonjwa asiyekusudiwa katika jamii.

Brosha hii inakupa maelezo kuhusu haki zako ni nini na unachoweza kutazamia kama upo na agizo la matibabu ya jamii.

### Kwa nini agizo la matibabu ya jamii lilifanyikwa?

Kama wewe upo na agizo la matibabu ya jamii (Fomu 5A) ni kwa sababu mtaalum wa magonjwa ya akili alikuchunguza na ameamuliwa kuwa:

- una ugonjwa wa akili unaohitaji matibabu,
- kuna hatari ya maana kwako mwenyewe au kwa mtu mwengine kama hupati matibabu,
- huna afya nzuri ya kutosha kuweza kuamua uamuzi kuhusu matibabu,
- huhitaji kulazwa hospitalini kupata matibabu, na
- hakuna njia yenye mipaka kidogo zaidi ya kukupa matibabu badala ya agizo la matibabu ya jamii.

### Agizo la matibabu ya jamii lina maana gani kwako?

Agizo la matibabu ya jamii lina maana kuwa unaweza kuendelea kuishi katika jamii (kwa mfano nyumbani au hosteli), lakini wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa na ukubali matibabu yaliyopangliwa kwa wewe.

Angalau mara moja kila mwezi utakuwa na uchunguzi na mtaalum wako wa magonjwa ya akili anayekusimamisha au mweledi mwengine, na uhudhurie ule. Lazima ufuate maagizo yote yaliyoagizwa na mtaalum wako wa magonjwa ya akili anayekusimamisha. Hayo yanaelezwa katika masharti ya agizo lako la matibabu ya jamii.

### Nini itatokea usipotii agizo?

Ukiwa hutii agizo lako, (kwa mfano huhudhurii miadi au hufuati mpango wako wa matibabu), na mtaalum wako wa magonjwa ya akili amechukua hatua yote ya maana kukusukuma ili utii, ndipo wewe umevunja agizo la matibabu ya jamii.

Mtaalum wako wa magonjwa ya akili atakupa ‘Notisi ya Uvunjaji’ kukuambia kwamba hujatii, na unachohitaji kufanya ili kutii.

Kama bado hutii unaweza kupelekwa ‘Agizo la Kuhudhuria’, ambalo litakuwa fomu ya kukuagizia kwenda mahali fulani, (kama zahanati au hospitali), kwa wakati fulani kwa matibabu yako. Kama bado hutii, afisa wa polisi au afisa wa usafiri anaweza kutumiwa kukuta na kukuchukua mahali utakapopewa matibabu.

### Agizo la matibabu ya jamii linaendelea kwa muda gani?

Agizo la matibabu ya jamii linaweza kuendelea kwa hadi ya miezi 3. Tarehe ya mwisho ya agizo itaandikishwa kwa Fomu 5A, na utapewa nakala.

Katika wiki ya mwisho ya agizo, mtaalum wako wa magonjwa ya akili anayekusimamisha ataamua kama agizo linahitaji kuendelea. Mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kuendeleza agizo kwa hadi ya miezi 3. Agiza la matibabu ya jamii linaweza kuendelea mara nyingi iwezekanavyo kuhitajika mpaka una afya nzuri ya kutosha kutohitaji matibabu yasiyokusudiwa.

Ukiwa hukubali kuwa agizo lako liendelee, unaweza kuomba mtaalum wako wa magonjwa ya akili kupanga maoni ziada na mtaalum mwengine wa magonjwa ya akili. Mtaalum wa magonjwa ya akili wa pili akuone katika siku 14 kuamua kwa vyovyote vile agizo kuendelea au la. Ikiwa unaomba kwa maoni zaida lakini huyapati, agizo haliwezi kuendelea (isipokuwa maoni ya ziada hayatoi kwa sababu hukuhudhuria miadi, na kwa kesi hiyo agizo linaendelea).

### Agizo la matibabu ya jamii aliyelazwa linaisha jinsi gani?

Agiza lako la matibabu ya jamii halitakufaa kama:

- linaisha na haliendelee, au
- wakati wowote, mtaalum wa magonjwa ya akili anaamua kuwa una afya nzuri ya kutosha ili agizo la matibabu ya jamii lifutwe, au
- mtaalum wako wa magonjwa ya akili anakuchunguza na anaamua kuwa unahitaji matibabu hospitalini, na anafanya agizo la matibabu ya mgonwa aliyelazwa, au
- Baraza ya Afya ya Akili inakagua kesi yako na inaamua kwamba huhitaji tena kuwa mgonjwa asiyekusudiwa.